# Wasafirishaji wapewa siku 14 tiketi mtandao

**DAR ES SALAAM**

NA MWANDISHI **WETU**

Serikali imetoa siku 14 kwa wasafirishaji wa mabasi ya ndani na nje ya nchi kuhakikisha wanajiunga na wenzao walioidhinishwa kutumia mfumo wa tiketi mtandao kutoa huduma hiyo, la sivyo wataondolewa sokoni.

Akizungumza na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA), Salum Pazzy, amesema agizo hilo linaanza kutekelezwa Januari 30 hadi Februari 15.

"Wamiliki wa mabasi wanaelekezwa kutumia mifumo ya tiketi mtandao iliyoidhinishwa pekee,wasafirishaji ambao sasa wameunganisha mabasi yao kwenye mifumo isiyoidhinishwa wanapewa muda wa siku 14 hadi Februari 15,mwaka huu kuhamia kwenye mifumo iliyoidhinishwa.

"Baada ya tarehe hiyo, hawataruhusiwa kutoa huduma kwa kutumia mifumo isiyoidhinishwa,kuanzia tarehe hiyo, utoaji na uhuishaji wa leseni za usafirishaji wa abiria utazingatia matumizi ya mifumo ya tiketi mtandao iliyoidhinishwa.

Amesema hadi Januari 30, mwaka huu mifumo 10 ya tiketi mtandao imekidhi vigezo vya kisheria na kuidhinishwa kuendelea kutoa huduma.

Kampuni na mifumo yao ya tiketi mtandao iliyoidhinishwa ni AB Courier Express Limited AB Connect, Busbora Company (Limited Busbora), Hashtech Tanzania Limited (MySafari tiketi), Iyishe Company Limited (Iyishe Company Limited) na Logix Company Limited (Msafiri).

Mingine ni Mkombozi Infotech Company (Baspoa), Otapp Agency Company Limited (Otapp), Sepatech Company Limited (Afritech), Voltic Tanzania Limited (Voltic Tanzania Limited) na Web Corporation Limited (Web e-ticketing).

Amezitaja kampuni ambazo zimeshindwa kukidhi vigezo kuwa ni Exabytes Africa Ltd (Exabytes Tiketi), Global Light & Company Limited (Tiketi Rafiki), Duarani Innovat Limited (Safari Yetu) na Itule Company Limited (Safiri Tiketi).

"Mifumo mingine yote ya tiketi mtandao tofauti na ile iliyotajwa hapo juu, imeshindwa kukidhi matakwa ya kisheria licha ya kupewa muda wa kutosha kurekebisha upungufu ulioainishwa kwa mujibu wa sharia. Mifumo hii haitambuliki na mamlaka na hairuhusiwi kuendelea kutoa huduma," amesema Pazzy.

Amesema kwa mujibu wa Kanuni ya 5 ya kanuni hizo, mfumo wa tiketi mtandao unaostahili kupewa kibali unapaswa kutimiza vigezo kama vile uwe unamilikiwa na taasisi ya serikali, chama cha ushirika au kampuni iliyosajiliwa Tanzania, uwe umeunganishwa na mfumo wa usimamizi wa malipo ya mapato wa kielektroniki, uwe una uwezo wa kuunganishwa na mifumo ya mamlaka, mfumo mkuu wa tiketi mtandao na mfumo wowote kama inavyohitajika.

Kutokana na hali hiyo, Pazzy amewasihi Watanzania kuendelea kukata tiketi kwa njia ya mtandao ili kuepuka usumbufu na utapeli unaoweza kufanywa na watu wasiokuwa na nia njema kwa abiria.

CamScanner

Jumanne February 3, 2026

# LATRA kuwawezesha maofisa usafirishaji

NJOMBE

NA MWANDISHI **WETU**

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kwa kushirikiana na uongozi wa Mkoa wa Njombe imeanza utekelezaji wa mpango wa kuanzisha Chama cha Ushirika (SACCOS) cha kwanza cha maofisa usafirishaji wa pikipiki na bajaji, hatua inayolenga kurasimisha shughuli zao na kuwawezesha vijana kujikwamua kiuchumi.

Hayo yamesemwa na Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, alipofanya kikao chake na Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, Dk. Habibu Suluo, alipofanya ziara mkoani humo kwa lengo la kukutana na kuzungumza na maofisa usafirishaji.

Mataka amesema wazo la mamlaka kuanzisha SACCOS ni kubwa na linakwenda kutoa suluhisho la muda mrefu katika sekta ya usafirishaji mkoani humo kwa vijana wengi ambao wanafanya kazi hiyo.

"Wazo hili litawezesha kazi ya bodaboda na bajaji kurasimishwa kama kazi nyingine kupitia SACCOS inayokwenda kuanzishwa, wasafirishaji wataweza kujiwekea akiba zao, kuongeza kipato na kupata huduma za bima kama zilivyo ajira nyingine.

"Serikali ya mkoa ipo tayari kushirikiana na LATRA kuhakikisha SACCOS itakayokwenda kuanzishwa inakuwa ya mfano wa kuigwa kitaifa na kuwa chombo muhimu cha kuwawezesha wasafirishaji kujikwamua kiuchumi," amesema Mtaka."

Kwa upande wake, Dk. Suluo amesema mamlaka imeweka mkakati maalumu wa kuwaangalia kwa karibu vijana wa sekta ya usafirishaji kwa lengo la kuboresha huduma za usafiri mkoani hapo.

"SACCOS hii inayoanzishwa Njombe itakuwa ya kwanza na ya mfano katika mkoa huu, mtazamo wetu ni kuwa na mfumo wa kidijiti utakaowaunganisha vijana wote wa usafirishaji - kuanzia ngazi ya mkoa, wilaya hadi kata, utakaowawezesha kujitambua, kupata taarifa zao kwa urahisi na hatimaye kuunganishwa katika mfumo wa kitaifa, hatua itakayoboresha huduma za usafiri na kuongeza uwajibikaji ili kupata ushirikiano wa pamoja," amesema.

Ameongeza kwamba sheria ya mamlaka imebaini umuhimu wa wasafirishaji wa pikipiki pamoja na bajaji kujiendesha na kujisimamia wenyewe, hivyo kupendekeza uwepo wa vyama vya ushirika ambavyo baada ya kupitishwa kwa kanuni husika, mamlaka imeendelea kutoa elimu na kuhamasisha uundaji wake.

"Kabla ya kuwapatia uwakala wasafirishaji wanawasilisha maombi, mamlaka kupitia Mfumo wa Usimamizi na Utoaji Leseni za Usafiri wa Barabara na Reli (RRIMS), tukiridhika vigezo vimetimizwa, wanaanza kufanya kazi kupitia mfumo. Mapato yao yanaingia kwenye mfumo wetu kupitia namba ya malipo (control number) na kila mwezi tunawarejeshea asilimia 20 ya mapato wanayokusanya," amesema.

Katibu Mtendaji Tume ya Taifa ya Mipango, Dk. Fredy Msemwa, amesema mpango wa kuanzishwa SACCOS unaendana na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, yenye lengo la kuchochea urasimishaji na kukuza sekta ndogo ya ushirika nchini.

CamScanner




# Feasibility study for Mbamba Bay SGR completed

THE government has completed the feasibility study and preliminary design for the construction of a 1,000-kilometre Standard Gauge Railway (SGR) from Mtwara to Mbamba Bay, including branches to Liganga and Mchuchuma, the National Assembly heard yesterday.

Deputy Minister for Transport David Kihenzile said the work was carried out through the Tanzania Railways Corporation (TRC) as part of ongoing efforts to expand the national rail network and support strategic economic projects.

He was responding to a basic question from Mtama MP Nape Nnauye (CCM), who asked whether the government intends to begin feasibility work for an SGR line from Dar es Salaam to the southern regions to serve the Liquefied Natural Gas (LNG) project.

Mr Kihenzile said the government is currently mobilising financial resources for the Mtwara–Mbamba Bay SGR, including exploring Public–Private Partnership (PPP) arrangements.

He added that the Dar es Salaam–Mtwara railway section has been recognised by the East African Community (EAC) under the East Africa Railway Master Plan due to its strategic importance in linking the two ports and promoting economic and regional integration.

"However, at present this section has not been included in government-funded projects," he noted.

The Deputy Minister said the government continues to implement major strategic projects, including the national SGR, in phases due to the substantial financial requirements involved.

He encouraged private investors and financial institutions to partner with the government in rail development, including the southern corridor, starting with updated feasibility studies.

In a supplementary question, Mr Nape asked whether the government was considering taking full ownership of the southern SGR project instead of relying on EAC frameworks, arguing that doing so could give Tanzania a competitive advantage in the region.

Responding, Mr Kihenzile said the project remains a national priority and that its inclusion in the EAC master plan was strategic.

"The aim was to secure regional prioritisation, enable joint mobilisation of resources for corridor projects and ensure alignment with other infrastructure being developed across the Community," he said.

The MP further sought clarification on whether the government was ready to partner with LNG investors, who stand to benefit from the railway for cargo transportation and project logistics.

Mr Kihenzile said the government recognises the central role of the private sector, noting that amendments to the Railways Act No. 10 of 2017 were made precisely to allow private participation in rail construction and operations.

CamScanner

Jumanne February 3 2026

UHURU
MAONI YA MHARIRI

# Usafiri reli za kisasa mijini umekuja wakati mwafaka

Ni habari nyema! Ndivyo unavyoweza kusema kufuatia taarifa za kukamilika kwa mchakato wa kuanza ujenzi wa reli za kisasa mijini.

Tunasema ni habari hasa ikizingatiwa umuhimu wa usafiri huo kwa majiji kama ya Dar es Salaam ambao una shughuli nyingi za kiuchumi na Dodoma ambao ndiyo makao makuu ya nchi.

Habari hizo njema zilitangazwa juzi na Waziri wa Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa, alipozungumza na waandishi wa habari, kuhusu mafanikio yaliyopatikana ndani ya siku 100 za uongozi wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Katika mkutano huo, Profesa Mbarawa alisema serikali imekamilisha upembuzi yakinifu wa ujenzi wa reli ya kisasa za mijini katika Jiji la Dar es Salaam na Dodoma.

Alisema hatua hiyo, inalenga kupunguza msongamano wa usafiri wa umma na kuongeza tija katika miji mikuu ya kiutawala na kibiashara nchini.

Kwa mujibu wa Profesa Mbarawa, Rais Samia, amewezesha kupatikana fedha za msaada kwa usanifu wa kina wa mradi huo, hatua itakayofungua rasmi utekelezaji wake.

Alisema hatua hiyo, imefungua fursa ya kupata fedha za msaada za usanifu wa kina, hatimaye utekelezaji wa mradi huo muhimu unaolenga kupunguza msongamano wa usafiri wa umma na kuongeza tija.

Tunampongeza Rais Dk. Samia kwa kufanikisha upatikanaji wa msaada utaowezesha mchakato ya ujenzi wa reli hiyo na serikali kwa kufanikisha maandalizi ya kuanza kwa mradi huo.

Ni ukweli usiofichika kwamba msomangano wa usafiri katika miji mikuu na kibiashara huchangiwa na miundombinu duni, kukidhi mahitaji ya wasafiri.

Jiji kama la Dar es Salaam na sasa Dodoma ni miongoni mwa majiji yanayokabiliwa na changamoto ya msongamono kutokana na kasi ya ukuaji wake.

Mfano Jiji la Dar es Salaam, mtu naweza kuchukua saa moja hadi mbili kutoka Kigamboni kufika kati kati ya Jiji kwa umbali wa kilomita zisizozidi 25.

Kadhia hii imekuwa ikikwamisha shughuli za kijamii na kiuchumi kutokana na watu kutumia muda mrefu wakiwa ndani ya vyombo vya usafiri kutokana na msongamano wa magari.

Aidha msongamano huo, umekuwa ukichangia serikali kupoteza mapato kutokana na shughuli za kiuchumi kukwama kutokana na watu kushindwa kufika kwa wakati kazini na kwenye shughuli zingine za kiuchumi.

Pia utoaji wa huduma zikiwemo za usafiri huathirika kutokana na msongamano wa magari yakiwemo malori yenye shehena za bidhaa kutoka bandarini na yale yenye nafaka na vyakula kutoka mikoani.

Mbali na kumaliza changamoto ya usafiri wa umma, reli za kisasa zitapunguza msongamano kwa kuwa baadhi ya wenyer magari wanaweza kuamua kutumia usafiri huo rafiki.

Pia usafiri wa reli mijini hupendezesha miji, sanjari na kupunguza uchafuzi wa mazingira kwa kupunguza msongamano wa magari barabarani.

Kimsingi ni mradi mzuri uliokuja wakati mwafaka kumaliza kero ya msongamano katika majiji yetu, ambayo ndiyo kioo cha nchi kutokana na kupokea wageni kutoka mataifa mbalimbali duniani.

Ni matarajio yetu hatua iliyofikiwa ni mwanzo mzuri wa ujio wa usafiri wa reli za kisasa katika majiji yetu, utakaopunguza adha ya msongamano barabarani na kupamba mandhari ya miji yetu.



CS CamScanner

NIPASHE Jumanne February 3, 2026

# Mwitikio abiria SGR washtua, serikali yaongeza mabehewa

> "Kwa sasa mishahara na uendeshaji wa TRC vinategemea makusanyo ya ndani, hatua inayoliongezea shirika uwezo wa kujiendesha kibiashara,"
> Prof. Mbarawa

**Na Rehema Matowo,** Dodoma

SSERIKALI imetangaza kuwa iko mbioni kuongeza mabehewa na vichwa vya treni kwenye reli ya kisasa (SGR) kutokana na ongezeko kubwa la abiria wanaotumia usafiri huo kati ya Dar es Salaam na Dodoma.

Imeelezwa kuwa kutokana na ongezeko hilo, baadhi ya wasafiri wanalazimika kukata tiketi siku tatu hadi tano kabla ya safari ili kupata nafasi.

Waziri wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, aliyasema hayo jana wakati akiwasilisha taarifa ya mafanikio ya siku 100 za Rais Samia Suluhu Hassan katika awamu ya sita, kipindi cha pili, akieleza kuwa mwitikio wa Watanzania kutumia SGR umevuka makadirio ya awali ya serikali.

Akijibu swali la mwandishi wa habari kuhusu mpango wa wizara kukabiliana na upungufu wa mabehewa, Prof. Mbarawa alisema serikali tayari imetambua changamoto hiyo na imeanza taratibu za kuongeza mabehewa pamoja na vichwa vipya vya treni.

"Tulileta mabehewa na vichwa vya treni vya kutosha kwa mujibu wa makadirio yetu, lakini abiria wamekuwa wengi zaidi ya tulivyotarajia," Waziri Mbarawa alisema.

Alibainisha kuwa hatua hiyo inalenga kupunguza usumbufu kwa wananchi, kurahisisha upatikanaji tiketi na kuwawezesha wasafiri kufanya shughuli zao za kijamii na kiuchumi kwa ufanisi zaidi.

Prof. Mbarawa alisisitiza kuwa SGR ni usafiri wa kisasa na wa haraka, akieleza kuwa Tanzania ndiyo nchi pekee katika Afrika Mashariki yenye reli ya mwendokasi inayofikia kilomita 160 kwa saa.

Safari ya Dar es Salaam hadi Dodoma, alisema, huchukua kati ya saa tatu hadi saa tatu na nusu, jambo linaloongeza mvuto wa huduma hiyo kwa wananchi.

Akizungumzia mafanikio mengine katika kipindi hicho cha siku 100, waziri huyo alisema wizara imepiga hatua kubwa katika kuimarisha reli ya TAZARA, baada ya kutia saini mkataba wa ufufuaji na uboreshaji kati ya Tanzania na Zambia Septemba 2025.

Alisema utekelezaji rasmi wa mradi huo unatarajiwa kuanza Juni mwaka huu, hatua itakayoongeza ufanisi wa Bandari ya Dar es Salaam, kuchochea biashara na kufungua fursa za ajira katika mikoa inayopitiwa na reli hiyo.


Kwa upande wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), Prof. Mbarawa alisema kuwa kuanzia Desemba 2025 shirika hilo limeanza kujitegemea kifedha, baada ya kwa zaidi ya miaka 13 kupokea ruzuku ya mishahara ya takribani Sh. bilioni 13 kwa mwaka.

"Kwa sasa mishahara na uendeshaji wa TRC vinategemea makusanyo ya ndani, hatua inayoliongezea shirika uwezo wa kujiendesha kibiashara," alisema.

Katika siku 100 zilizopita, TRC imesafirisha jumla ya abiria 838,870, ambapo asilimia 89 walitumia SGR na asilimia 21 walitumia reli ya MGR, hali inayoonesha mafanikio makubwa ya uendeshaji reli nchini.

CamScanner

# Mara inavyopambana kutoa elimu kwa madereva wa bodaboda



Pikipiki zikiwa zimepangwa sehemu moja mjini Bunda mkoani Mara, wakati madereva wakiwa katika mafunzo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

- Lengo ni kila mmoja apate ujuzi
- Gharama za leseni zapunguzwa

**Na Sabato Kasika**

TASNIA ya boda boda ni uti wa mgongo wa uchumi wa usafiri na usafirishaji unaohusisha zaidi ya madereva 10,000 ambao wana ajira za moja kwa moja za vijana.

Lakini pia wapo wengine mamia wanaonufaika na kuuza vipuri, kofia, kuzisambaza na kuzikarabati pikipiki hizo.

Anaeleza Mkuu wa Mkoa wa Mara, Kanali Evans Mtambi, anayefafanua kuwa maelfu ya familia mkoani humo hupata chakula cha kila siku kupitia biashara ya bodaboda.

Ni biashara ambayo pengine huwaingizia wastani wa Shilingi 20,000 kila leo zinazotunza familia zao na wategemezi wao.

Mkuu wa Mkoa anawaona boda wakichangia kodi kila siku, kuanzia kwenye ushuru wa mafuta hadi kwenye usajili kupitia ada na leseni na pia wanaimarisha mifumo ya fedha kwa kukopa mikopo ya halmashauri ya asilimia 4:4:2

"Kazi ya udereva wa bodaboda ina umuhimu mkubwa katika jamii na uchumi wa nchi ni ajira, hurahisisha usafiri na usafirishaji kufika haraka katika maeneo ambayo magari hayafika kirahisi," anaeleza.

Mkuu huyo wa mkoa anasema usafiri huo haufanikiwi bila kuwapa madereva mafunzo maalumu kupunguza ajali na vifo barabarani, kwa kuwa ajali nyingi za bodaboda huchangiwa na sababu mbalimbali ikiwamo kutojua sheria za barabarani, mwendo wa haraka na kutovaa kofia ngumu.

Katika mazungumzo yake na gazeti hili Kanali Mtambi anasema mkoa unakadiriwa kuwa na madereva wa bodaboda zaidi ya 10,000 serikali imeanzisha mpango wa kuwapa mafunzo kwa lengo la kuwajengea uelewa ili kupunguza ajali.

"Mkoa wa Mara una zaidi ya madereva 10,000 wa boda ambao wote watapata mafunzo ya udereva kutoka kwa wakufunzi wa Chuo cha Ufundi Stadi (VETA)," anasema Kanali Mtambi.

Mafunzo yanafanyika kila wilaya, na kwamba tayari madereva wa manispaa ya Musoma, wilaya za Tarime na Bunda wameshaingizwa darasani na wataendelea katika wilaya nyingine, anasema.

"Madereva wa wilaya za Buatiama, Serengeti, Rorya na Musoma watapata mafunzo hayo, lengo letu ni kila dereva wa bodaboda afundishwe ujuzi wa kufanya kazi hiyo," anasema.

unasaidia kuokoa muda, hasa maeneo yenye msongamano wa magari na kusaidia wananchi kuwahi katika shughuli zao na kupitia kazi hiyo, fedha huzunguka katika jamii na kuchangia ulipaji kodi na kuchochea biashara ndogo na kupunguza ukosefu wa ajira.

### WANACHOTARAJIA

Ni pamoja na madereva kujua sheria, kutambua na kuziheshimu alama za barabarani, mbinu sahihi za kuendesha pikipiki, kuepuka ajali au kupunguza zinazosababisha vifo na majeruhi.

"Dereva aliyesomea anajua kuendesha kwa tahadhari, kudhibiti mwendo, na kufanya maamuzi sahihi. Hivyo, anaweza kupunguza ajali, uharibifu wa pikipiki na gharama za matibabu," anasema.

Anafafanua kuwa katika udereva, kuna taaluma na nidhamu kazini, na kwamba elimu humjenga dereva kuwa mtaalamu, anayeheshimu abiria, anayevaa kofia ngumu na anayefuata maadili ya kazi.

Mbali na hayo, anasema kusomea kazi hiyo kunaongeza uelewa wa haki na wajibu, na kwamba madereva wanajua haki zao kisheria, wajibu wao na adhabu zinazohusiana na uvunjaji wa sheria.

"Madereva waliopita chuoni, huchangia usalama wa jamii, hupunguza mzigo wa ajali hospitalini, huleta heshima kwenye kazi ya bodaboda na pia mafunzo ya udereva yanaweza kusaidia kupata leseni sahihi, mikopo, ajira bora, au kujiendeleza katika kazi nyingine za usafirishaji." Anasema Mkuu wa Mkoa.

Anasema kila dereva wa bodaboda anatakiwa kuwa na leseni halali, kwa maelezo kwamba serikali imepunguza gharama za leseni kutoka Sh. 60,000 hadi 20,000, kwa ili kuwapa unafuu.

"Pamoja na hayo, madereva wanatakiwa kujiunga na vikundi kupitia vijiwe na kubuni biashara mbadala zikiwamo za ufugaji samaki kwa kutumia vizimba, nyuki, mifugo na maduka ili kujiongezea kipato na kujikwamua kiuchumi," anasema.

Katika kufanikisha uanzishwaji wa miradi, anawataka wakurugenzi wa kila halmashauri kusimamia utoaji wa mikopoy 4:4:2 na pia kutafuta wahisani ili kuwawezesha vijana waimarishe shughuli zao.

### VETA KUFANIKISHA

Mkuu wa Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), Mkoa wa Mara, Martin Mollel, anasema maofisa usafirishaji wa bodaboda hawana budi kuchangia fursa na kushiriki mafunzo kikamilifu ili kupata elimu na leseni kwa gharama nafuu.

Anasema licha ya wengi wao kuwa na ujuzi wa kuendesha vyombo vya moto, wanakosa mafunzo ya jinsi ya kutoa huduma bora kwa wateja, alama za barabarani na sheria za usalama pia.

"Mafunzo yanawajengea uwezo katika maeneo hayo, kuboresha ustawi wa jamii na kuongeza ubora wa huduma wanazotoa ili kujikwamua kiuchumi, hivyo suala la mafunzo ni muhimu," anasema Mollel.

Watakuwa watii wa sheria bila shuruti, kuimarisha usalama ndani ya mkoa huo, pia kuwa na leseni badala ya kuendelea kujificha na kukwepa kupata ujuzi kutoka VETA.

Ofisa Habari wa Umoja wa Madereva wa bodaboda mkoani humo, Faustine Mbaruku anasema wana kazi ya kuendelea kuhamasisha madereva hao kufahamu umuhimu wa kupata mafunzo hayo.

"Kwanza tunashukuru kwa kutupunguzia gharama za kupata leseni, kwa sababu tunaambiwa kuwa kiasi kingine cha fedha kitalipwa na serikali. Hii ni wazi kwamba inatutakia mema," anasema Mbaruku.

Anafafanua kuwa mchakato mrefu wa kupata leseni umekuwa ukisababisha wengi wao kufanya kazi bila leseni na kwamba njia ambayo serikali imeitumia itarahisha wengi wao kuzipata.

"Tumesogezewa elimu ya udereva salama na kuzijua sharia za usafirishaji. Madereva wote hatuna budi kuipata ili kufanya kazi yetu kwa weledi, lakini zaidi ni kwamba tumepunguziwa gharama ya kupata leseni, n wajibu wetu kutoikosa fursa hii," anasema.

CamScanner